

**HISTORIA FUPI YA UTAWALA WA  
KISASA WA KIMANGI NA  
'KATIBA' YAKE KASKAZINI MWA  
TANZANIA, 1945 -2000**

**Na Dr. Catherine Baroin**

[Historia hii imetafsiriwa kutoka kwa: BAROIN, Catherine. 2003. A brief history of a neo-traditional form of chieftaincy and its 'constitution' in Northern Tanzania, 1945-2000. In: Wim van BINSBERGEN, in collaboration with Riekje PELGRIM (ed.), *The Dynamics of Power and the Rule of Law. Essays on Africa and beyond in honour of Emile Adriaan B. van Rouveroy van Nieuwaal*, Leiden: African Studies Centre, pp. 151-166.]

## Utangulizi

Van Rouveroy van Nieuwaal amekua akisisitizia mara kwa mara kwamba viongozi wa kimila wa Kiafrika wamekuwa wakitumika kwa njia tata yenye sehemu mbili tofauti: kwa upande mmoja wako katikati ya dola na serikali yake ambapo wanapaswa kuhakikisha sera na sheria za nchi zinatekelezwa ipasavyo; na kwa upande mwingine wanawajibika kimila kwa watu wao wanaowatawala ambapo sehemu hizi mbili zaweza kuwa na misimamo au maslahi tofauti na yanayopingana katika masuala mbalimbali ya kimsingi. Hata pale ambapo wanapoonekana kutotaka kuwa vibaraka wa moja kwa moja wa kufuata mfumo wa kiserikali, au wakati ambapo mfumo wa kisiasa katika jamii unaporuhusu mabadiliko fulani bado viongozi hawa wa kimila wanajikuta wamenasa njia panda wakibakia kuunganisha hali hizo mbili na nafasi zao kwa njia isiyoepukika.<sup>1</sup>

Hadi mwazoni mwa miaka ya 1950 watawala wa kimila (mangi) wa Wameru wanaopatikana Kaskazini mwa Tanzania walikuwa wakipitia katika mfumo huu tata wa utawala.<sup>2</sup> Madhalani, ugomvi wa ardhi baina ya Wameru na serikali ya kikoloni ya Waingereza ulibainisha wazi aina hiyo ya utata wa viongozi wa kimila kati ya kutii serikali ya kikoloni au watu wao, na hatimaye kulitokea chuki kati ya viongozi hao wa

---

<sup>1</sup> Angalia Van Rouveroy van Nieuwaal 1992, 1996, 1999.

<sup>2</sup> Tanzania ilizaliwa Mwaka 1964 kutokana na Mungano wa Tanganyika na Zanzibar.

kimila wa Kimeru na watu wao. Hali hiyo ilipelekea utawala huo kuondolewa na nafasi yao kuchukuliwa na mfumo tofauti na mpya wa kiutawala wa kimangi. Baadaye majukumu ya utawala wa kimila ya hapo awali yakagawanyika sehemu mbili. Awali kabisa kulikuwa na mtawala wa kimila aliyejulikana kama Mangi ambaye alikuwa akitambulika na utawala wa kikoloni na ambaye kiuhalisia alikuwa na mamlaka kidogo. Kwa upande mwingine kukawa sasa na mtawala mkuu (*Nshili Nnini*) ambaye hakuwa rasmi kwa utawala wa kikoloni, ambaye alihusika zaidi na mambo ya kimila katika kabila lake. Huyu alionekana kama sio kiongozi rasmi lakini kiukweli alikuwa ndiye msimamizi mkuu wa mila za Wameru. Historia hii kimsingi inaelezea mifumo hii ya kiutawala ambayo Wameru wameipitia mpaka sasa, ambayo mpaka leo hii imekuwa na umuhimu mkubwa sana kwa Wameru kuanzia kwa mtu binafsi au jamii kwa ujumla.

### **Historia ya Nyuma (1947-1953)**

Kihistoria Wameru (Varwa) ni wakulima wa Kibantu ambao walikuwa wakilima katika maeneo yenye rutuba katika miteremko ya kusini mwa Mlima Meru (wa urefu wa mita 4585). Kama takribani kilomita 50 hivi kwa upande wa Mashariki kuna ndugu zao Wachaga wa Kilimanjaro.<sup>3</sup> Kama

---

<sup>3</sup> Angalia Moore 1986.

ilivyo kwa Wachaga, Wameru waliotesha migomba na kahawa zikiwa zimechanganyikana na mahindi pamoja na maharage ambapo mazao hayo yalikuwa yakipandwa chini ya miteremko ya mlima huo. Katika mwaka 1930 hadi 1940 Wameru waliweza kuongezeka kwa kasi, jambo lililopelekea kuwa na kubanana katika ardhi miongoni mwa jamii yao na hata walowezi wa Kikoloni. Hali hii ilitokea baada ya walowezi wa Kizungu kuanzisha mashamba makubwa ya kahawa katika maeneo ya Wameru hali iliyowazuia Wameru kuenea katika maeneo ya kusini mwa Mlima Meru kwa ajili ya malisho ya mifugo yao na maeneo yenye maji.<sup>4</sup>

Katika kaskazini mwa Tanganyika, utawala wa Kiingereza uliweza kutafuta suluhisho la kudumu juu ya migogoro ya mara kwa mara ya ardhi baina ya walowezi wa Kizungu na Wameru, ambapo waliunda Kamati ya kitaalamu iliyoongozwa na Justice Wilson ili kufanya uchunguzi juu ya mizozo hiyo. Yeye aliamini kwamba Waafrika ni watu wa kulima mazao mbali mbali ambayo siyo ya biashara na kuwa vibarua katika mashamba ya walowezi na pia kuwa nguvu kazi katika sekta nyingine za uchumi, ambapo walowezi wa Kizungu wao wangejishughulisha na kuanzisha mashamba makubwa ya

---

<sup>4</sup> Iliffe 1979: 145; Luanda 1986: 273 na ramani III. Na Wameru hawakuwa wenyewe katika hali hiyo. Jirani zao huko Kenya, Walowezi Weupe na Wakulima wa Ki-Afrika walipigania ardhi; huko Kikuyu mzozo ulisababisha kukwama kwa Serikali mwishoni m wa miaka ya 1940 na hata kukatokea vita ya Mau Mau mwaka 1952 – 1956. Kwa Wachagga wa Mlima Kilimanjaro, jirani ya Wameru, kwa upande wao hali ilikua shwari kwani mashamba ya Wazungu yaliyowazunguka hayakuwa na mvuto sana.

kahawa.<sup>5</sup> Wilson alitetea kuenea na kupanuka kwa mashamba ya walowezi wa Kizungu na hivyo wakayapora zaidi mashamba na malisho ya Wameru hasa kwa upande wa mashariki mwa Mlima Meru. Wameru ambao tokea hapo awali walikuwa wamebanana katika maeneo yao madogo ya mlimani nao tayari walitaka kupanua kilimo chao cha kahawa. Hivyo walianza kupinga uporaji huu wa ardhi yao ya asili. Upinzani dhidi ya kuenea kwa Ukoloni katika maeneo yao uliongozwa zaidi na vijana waliosoma wa Kikristo ambao pia walikuwa wakulima wa kahawa waliojua kusoma na kuandika baada ya kupitia shule za misioni za Kanisa la Kilutheri na baada ya kupata ujuzi wao wa kielimu walitaka sasa kupata ushawishi mkubwa katika jamii yao.<sup>6</sup>

Wakati wa mwazoni mwa miaka ya 1940, Tanganyika ilikuwa katika nafasi ya pekee sana katika dola ya Kiingereza. Iliwekwa chini ya udhamini wa Jumuiya ya Kimataifa [League of Nations] ambapo baada ya Ujerumani kushindwa katika vita ya kwanza ya dunia, ilivekwa chini ya uangalizi wa Uingereza.<sup>7</sup> Hivyo basi, Waingereza walikuwa na uwezo wa kisheria na kiutawala hapa nchini ingawa walikuwa wamebanwa kuipa kipaumbele nafasi ya Waafrika na kukuza maendeleo yao na ustawi wao katika nyanja mbali mbali

---

<sup>5</sup> Spear 1997: 216.

<sup>6</sup> Baroin 1998: 538-541.

<sup>7</sup> Makubaliano hayo yalipitishwa rasmi baadaye na Jumuiya ya Umoja wa Mataifa.

kiuchumi na kijamii.<sup>8</sup> Kwa misingi hiyo Waingereza wakajaribu kuanzisha sera mpya ya utawala wa wazawa ambapo mamlaka zao za awali [Native Authorities] zilibadilishwa na kuwa na mfumo wa kisasa na wa kidemokrasia. Kwa mujibu wa utawala wa Kikoloni, ilisemekana kuwa viongozi wa kimila wachaguliwe kwa kupigiwa kura na kuongoza kwa kutumia katiba iliyoandikwa na kabila husika, mfumo ambao ungeenda sambamba na taratibu za kisasa za kiutawala kama vile mgawanyo wa madaraka katika mihimili ya bunge na kiserikali.<sup>9</sup>

Mnamo mwaka 1948, mazungumzo juu ya kutengeneza katiba za kikabila yalianza. Kutokana na kuongezeka kwa hali ya mashaka katika eneo la Mlima Meru, Wameru walikataa kabisa kujiunga na mazungumzo hayo. Walimpinga kiongozi wao wa kimila (Mangi) kwa kuwa walidhani alikuwa akiunga mkono utawala wa kinyonyaji wa Wazungu. Hivyo walimtaka ajiuzulu. Waingereza walijaribu kupambana na uasi huo kwa kuwapeleka kizuizini baadhi ya viongozi wa maasi hayo lakini hali ikazidi kuwa mbaya zaidi. Mangi alipozidi kujiimarisha katika utawala wake, hali ya mashaka ilizidi kutanda na mamia ya Wameru walijiunga na Umoja wa Watu wa Kilimanjaro (KCU), chama kipya cha kisiasa kilichokuwa kimeanzishwa na Wachaga mwaka uliopita na kilichokuwa na malengo ya

---

<sup>8</sup> Iliffe1979: 246-247.

<sup>9</sup>Cory makala namba 71.

kuvuruga mfumo wa tawala za kimila za Wachaga.<sup>10</sup> Pamoja na upinzani mkali wa Wameru, Katiba iliundwa na kukubalika ingawaje haikuweza kuwekwa kwenye utekelezaji.<sup>11</sup>

Mwaka 1951 unakumbukwa sana katika historia ya Wameru. Huu ndio mwaka ambao Wazungu walipora kwa nguvu ardhi ya Wameru, ambapo baya zaidi Waingereza walithubutu kuchoma moto Kanisa la Kilutheri la wazawa, mahali ambapo palikuwa pa muhimu sana kwa Wakristo wa Kimeru waliokuwa na msimamo na imani dhabiti. Matukio mengine mabaya yaliyoacha madhara makubwa yalitokea wakati huo huo ikiwa ni muendelezo wa tukio hilo.

Mnamo tarehe moja mwezi wa kwaza, Wameru walijipanga na kuandaa mapambano kupitia chama huru kilichojulikana kama Meru Citizens Union (MCU) ambacho kilimeguka kutoka chama kile cha Wachaga cha Kilimanjaro Citizens Union. Chama hiki kilikuwa na mchango mkubwa sana hasa katika mapambano dhidi ya utawala wa Kiingereza na katika kuunda ushirika huru wa wakulima wa kahawa.

Mnamo tarehe 24 mwezi wa pili, Wameru walichagua kiongozi wao wa kwanza wa kuwaongoza, ikiwa ni sambamba na Mangi aliyeungwa mkono na Waingereza. Mtawala huyu wakampa jina *Nshili Nnini*, yaani kiongozi mkuu, jina ambalo tokea hapo awali lilitumika likiwa na maana ya kiongozi wa

---

<sup>10</sup> Iliffe 1979: 491-494.

<sup>11</sup> Utawala wa Tanganyika, Taarifa Kuu ya Mwaka 1948, ukurasa wa 63.

ukoo yaani *Nshili wa Ufwari*. Wakati uchaguzi wa kiongozi mkuu katika hali hiyo iliyokuwa rasmi sasa ukifanyika, Kilimanjaro Citizens Union pia ilifanya kampeni ya kumchagua kiongozi mkuu wa Wachaga <sup>12</sup> wote ambapo Mangi Thomas Marialle alichaguliwa kuwa kiongozi mkuu wa Wachaga wote katika Mlima Kilimanjaro mwaka mmoja uliofuata. Hata hivyo uchaguzi wa *Nshili Nnini* wa Wameru haukutambulika na utawala wa Kiingereza. Uchaguzi huo kwa mfano haukuripotiwa katika ripoti ya mwaka ya Mkuu wa Wilaya (DC) jambo ambalo halikuwashangaza sana watu kwani hata hivyo utawala wake ulipingwa sana na Wameru. Hata hivyo tofauti hizo hazikuleta vita bali zilitumika ngazi za kiutawala na kisheria ila hata hivyo kulikuwa na mawasiliano ya kimataifa ili kuhakikisha suala hilo la Wameru linafahamika duniani kote.<sup>13</sup> Mkuu wa Wilaya (DC) wa Kiingereza asingeweza kuzisifu jitihada hizi za Wameru kama kabila.<sup>14</sup>

Baadaye kidogo Wameru walimkodisha mwanasheria na kufungua kesi dhidi ya Waingereza, kesi ya Wameru ilisikilizwa katika Baraza la Udhamini la Umoja wa Mataifa, ambalo ndilo lililokuwepo hapo awali kabla ya kuanzishwa rasmi kwa Umoja wa Mataifa huko New York mnamo mwaka 1952. Hii ilikuwa ni mara ya kwanza kwa kabila moja dogo la

---

<sup>12</sup> Moore 1986: 154.

<sup>13</sup> Spear 1997: 223.

<sup>14</sup> Ripoti ya Mwaka 1949 iliwataja Wameru kama kabila dogo lenye ushawishi mkubwa wa kisiasa kuliko lilivyodhaniwa.



Kiafrika kutoa changamoto kwa utawala wa kikoloni katika ngazi za Kimataifa na hivyo kujulikana sana katika historia ya mapambano dhidi ya ukoloni Barani Africa.<sup>15</sup> Hata hivyo mifumo mipya ya kiutawala na kimapambano iliyoanzishwa na Wameru baada ya kesi hii haijawahi kutajwa au kuripotiwa katika rekodi za Kikoloni au hata kutiliwa mkazo katika masomo au tafiti za baada yake.<sup>16</sup>

### **Mifumo mipya ya Kiutawala**

Utawala mpya ulioundwa na Wameru mwaka 1951 ulijumuisha sehemu kuu tatu:

- i. *Nshili Nnini*, au Kiongozi Mkuu.
- ii. Kamati<sup>17</sup> au Baraza Kuu.
- iii. Katiba ya Kabila.

Kazi kubwa ya viongozi hao ilikuwa ni kusimamia mambo ya kimila na kusimamia maadili na mambo ya kijamii kwa njia tofauti kabisa na mifumo ya kiutawala ya nchi. Serekali ya kikoloni ya Waigereza na baadaye serikali ya Tanzania hawakuingilia mambo haya ya ndani ya kabila. Ngoja tuangalie kwa undani mifumo hii mitatu ya utawala mpya wa Wameru.

---

<sup>15</sup> Japhet na Seaton 1967; Iliffe 1979; Spear 1997.

<sup>16</sup> Hata utafiti wa Puritt juu ya Wameru (1997); wala Kitabu cha Spear (1997) hawataji harakati hizo.

<sup>17</sup> Neno hili la Kiswahili lilipokelewa kutoka neno 'committee' la Kiingereza.

(i) *Nshili Nini* wa Wameru, huyu ndiye kiongozi mkuu wa kimila wa Wameru. Kwa Kiswahili huyu huitwa Mweyekiti wa koo zote Wameru, au Mwenyekiti wa mila wa Kabila la Wameru. Baadaye Wameru walimtafsiri kiongozi huyu kama Mwenyekiti mkuu wa Mila na Tamaduni za Wameru.<sup>18</sup> Kazi kuu ya *Nshili Nnini* ilikuwa ni kusimamia sheria za kimila kulingana na matakwa ya katiba. Hakutoa maamuzi peke yake, bali maamuzi yalifanywa kwa pamoja na hasa katika vikao, na mambo yote yalijadiliwa katika ngazi ya ukoo au katika mkutano mkuu wa *vashili* wote.

*Nshili Nnini* wa kwanza ambaye alichaguliwa tarehe 24 mwezi Februari 1951, alikuwa ni Tobia Nassari Ayo, aliyekuwa kiongozi wa ukoo wa Ayo. Ukoo wake ulikuwa ni wa kawaida na mdogo tu, na Tobia hakuchaguliwa kwa sababu ya utajiri au cheo bali kwa sifa zake binafsi. Alikuwa ni mstaarabu na mpole, aliyewasilikiliza watu na kuongea kwa busara. Alikuwa ni mtu mwenye maadili na anayefuata mila za Kimeru na utamaduni vizuri. Aliendelea kuwa *Nshili Nnini* kwa miaka 25, mpaka 1976, ambapo alijiuzulu kwa sababu ya uzee. *Nshili Nnini* aliyefuata alikuwa ni Yesaya Lemera Kaaya, aliyekuwa msaidizi wa Tobia kwa kipindi kirefu. Naye pia alijiuzulu kwa sababu ya umri mkubwa mwaka 1984. Moses Isacki Nnko, aliyekuwa kiongozi wa ukoo wa Nnko, aliichukua nafasi hiyo

---

<sup>18</sup> Tafsiri hii ni zaidi ya kuwa kiongozi wa jadi bali mlinzi wa taratibu za mababu, vizazi, asili na uadilifu (Johnson 1990: 147)

na alisimikwa mwezi Januari 1986. Huyu alijiuzulu mwaka 1994 sababu ya maradhi yaliyokuwa yakimsumbua na msaidizi wake Bethuel Paulo Kaaya akachaguliwa kuchukua nafasi hiyo.

*Nshili Nnini* na viongozi wa ukoo hawakuwa na mavazi rasmi. Walikuwa wanavaa nguo za kimagharibi kama watu wengine. Hata hivyo kikazi walitambuliwa kwa fimbo yao maalumu waliokuwa wakiishikilia. Kila *Nshili* alikuwa na fimbo yake hiyo maalumu iliyoitwa *Ndata*.<sup>19</sup> Ilikuwa na urefu wa sentimita 50 na mwishoni ilikuwa na umbo la tufe lenye ukubwa wa ngumi katika upande mmoja. Imekatwa katika mti mweusi na mgumu uitwao *senifu*. Kila *Nshili* alishika fimbo hiyo chini ya tufe na kuiweka wima. Hakuna mtu mwingine aliyeruhusiwa kushika fimbo hiyo. Ingawa *Nshili* aliweza kumlaani mtu afe kwa kumnyooshea fimbo hiyo au kwa kuigeuza juu chini mbele ya mtu huyo, hakutakiwa kuifanya fimbo yake kama kitu cha kuuwa mtu mwingine. Nguvu asilia ya fimbo hiyo (*ndata*) iliweza kuzuia mapigano. *Nshili* alitakiwa tu kuinyanyua juu mbele ya wanaogombana nao wataacha mara moja.

(ii) *Nshili Nnini* husimamia Baraza la *Washili* lililojulikana kama *Kamati*<sup>20</sup> ambalo kwa kawaida lilikuwa na wajumbe 15

---

<sup>19</sup> Fimbo hiyo ilitambulisha hadhi ya mtu na ilitumiwa pia na Wamasai na pia baadhi ya Waswahili.

<sup>20</sup> Kikao cake hujulikana kama Mringaringa, jina la mti mkubwa (*cordia abyssinica*, borag), ambapo ni mahali pa vikao, kijijini Poli.

mpaka 20 hivi, wakiwemo *Vashili* wa koo kubwa, makundi ya rika kubwa,<sup>21</sup> pamoja na wazee wa heshima katika kabila. Mwandishi, *katibu*<sup>22</sup> wa *Kamati* aliratibu vikao na kuandika yote yalioamuliwa na *Kamati*. Naye *Nshili Nnini* alikuwa na msaidizi wake (*ivele* au *ngoviri*). Msaidizi huyo kwa sababu ya uzoefu wake mara nyingi ndiye aliyekuja kuchaguliwa kuwa mrithi wa *Nshili Nnini*.

*Kamati* ilikuwa ikifanya vikao vyake mara mbili au tatu kwa mwezi, kujadili mambo mbalimbali ya kikabila. Kazi zao nyingi zilikuwa ni kujadili suluhu za migogoro (kama vile kesi ya ardhi ya Wameru wakati huo), kuratibu sera na michango kwa ajili ya maendeleo, ambapo pia ilifanya kazi kama mahakama kuu kwa kutatua migogoro ambayo haikupata muafaka katika ngazi za chini.

Ugomvi ulipojitokeza ulishughulikiwa kwanza katika ngazi za chini, kama vile familia ikiwa ni tatizo la kifamilia. Ikiwa ni ugomvi wa ukoo basi ulitatuliwa katika ngazi ya ukoo. Kama ni koo mbili zinahusika, viongozi wa koo hizo mbili wanakutana na kutatua tatizo hilo. Ni pale tu ambapo makubaliano hayakufikiwa katika ngazi za chini ndipo tatizo linapopelekwa katika ngazi za juu zaidi. Kama migogoro ya kifamilia haijatatuliwa na kiongozi wa familia, basi ilipelekwa

---

<sup>21</sup> Jamii ya Wameru imepangwa kulingana na umri wa wanaume wake wanaogawanywa kwenye marika, vijana wadogo huanza kwa kuingia katika rika dogo, na baada ya kama miaka 15 hivi huamia katika rika la vijana kupitia jando chini ya uanaglizi wa baba wa rika, na baadaye hulala kama wazee wa jamii hiyo.

<sup>22</sup>Neno la Kiswahili.

katika ngazi ya ukoo, na endapo ukoo nao ukishindwa kuutatua mgogoro huo basi ngazi ya juu zaidi kama *Kamati* itakaa ili kuutatua mgogoro huo. Hapo mwanzoni, mtu aliyepeleka shauri ili kutatuliwa alitakiwa kutoa pombe kama kinywaji cha kikao kwa wajumbe hasa wazee ili waweze kukaa na kutatua kesi hiyo. Lakini matumizi ya pombe yalipokatazwa hasa na Kanisa (Walutheri),<sup>23</sup> wajumbe au wazee walidai malipo ya aina nyingine toka kwa mshitaki yakiwemo vinywaji vingine au pesa kila walipokutana na kujadili kesi hiyo.

Ukiachana na matatizo yaliyoikumba jamii nzima, kesi ambayo inapelekwa kwa *Kamati* au *Baraza* ni ile ambayo inatokana na matatizo yanayoikumba jamii kila siku na imeshindikana kutatuliwa. Kesi nyingi zilihusiana na ardhi ambayo hujulikana kama mali ya ukoo, nyingine ni za urithi, kukodi au kuuza ardhi na kuharibu mipaka (kwa mfano mkulima anaweka mpaka wa shamba akizidisha na kuingia kwenye shamba la jirani yake). Matatizo ya kifamilia na ndoa nayo pia yalichukua muda katika agenda ya *Kamati*. Pia ugomvi baina ya mke na mume, wazazi na watoto, au maamuzi juu ya wajane na yatima. Yote haya yalichukuliwa sio matatizo ya mtu binafsi bali ni ya jamii nzima kwa ujumla wake. Pia fidia au malipo ya wizi, majeraha au mauaji nayo pia yaliletwa kwenye *Kamati*, na haya yalikuwa matatizo ambayo wanarika

---

<sup>23</sup>Baroin 2001: 89-92.

au ukoo walikuwa wanakumbana nayo kila mara. Nyingine zilikuwa ni kesi zinayohusiana na wanawake (kwa mfano mtu akitembea na mke wa mtu mwingine), au kutotimiza mikataba ya kukodishiana mifugo, ambazo zilipangiwa siku ya kusikiliza na kutatuliwa kwa sheria maalumu.

Kabla *Kamati* yote haijakutana kujadili tatizo, njia rahisi huwa inatafutwa, kwa mfano mjumbe mmoja au wajumbe wachache wataombwa kipekee kujaribu kwanza kutatua tatizo ambalo pande zinazohusika hazijaweza kuhafikiana ambapo inatumainiwa kuwa busara na mawazo ya wachache hao vitasaidia kufikia makubaliano. Kama suluhu haikupatikana, basi *Kamati* nzima itakutana kujadili tatizo hilo, na maamuzi au utatuzi mara nyingi hufikiwa. Watu huyaheshimu sana maamuzi ya *Kamati*, na si mara nyingi mtu huamua kupeleka kesi yake katika mahakama ya kiserikali. Hata ikiwa hukumu ya mahakama ya mwanzo kwa jambo fulani haikwenda sambamba na mila na desturi basi inaweza kurudishwa kwa *Kamati* ili kushughulikiwa. Moore akitoa maoni juu ya sheria za Kichaga aligundua kuwa zina mfumo sawa na Wameru, mifumo ambayo ni ya asili ya jamii ya watu jambo ambalo ni kinyume na sheria za kimahakama ambazo zinaegemea zaidi mifumo ya sheria za nchi za Magharibi. Sheria hizi za kimahakama zenye asili ya watu wa Ulaya huiona jamii kama bahari kubwa ya mtu mmoja mmoja na ambapo ukoo na familia

hazijapewa mtizamo wowote maalumu.<sup>24</sup> Hata hivyo ukweli unabaki kuwa kwa Wachaga na Wameru siku hizi familia na ukoo ni muhimu zaidi kuliko matakwa ya mtu binafsi. Familia na ukoo vimebaki kama muhimili mkubwa wa kijamii hata katika ngazi ya serikiali (iwe kwa Wachaga au kwa Wameru). Kwa sababu ya kushughulika na tatizo kwa njia maalumu inayojumuisha wadau wengi kama vile kuanzia ngazi ya ukoo, basi *Kamati* mara nyingi hufanikiwa katika kutatua matatizo yanayoletwa kwake.

Kuna kitu kimoja kingine cha kipekee ambacho kipo ndani ya uwezo wa *Kamati* ya Wameru, ambacho ni hukumu kwa njia ya kiapo. Na katika hili nitazungumzia suala la ‘kuvunja chungu.’<sup>25</sup> Huu ni utamaduni ambao unatumika mpaka sasa katika maisha ya Wameru kama njia ya kutatua mgogoro ikiwa njia nyingine zote zimeshindikana. Kama kuna uharibifu umetokea, ghala la mtu limechomwa, ng’ombe wameibwa, kipande cha mali (kama kesi ya 1997) kwa mfano redio ikiibwa kwenye nyumba, na ikiwa uchunguzi wa kina umefanyika na hakuna mwizi au mwovu ambaye amepatikana, basi kuna njia moja tu ya muhimu ya kupata malipo au kulipiza kisasi, ni kuitisha taratibu za tambiko liitwalo ‘kuvunja

---

<sup>24</sup> Moore 1986: 169.

<sup>25</sup> *Ipara nungu* kwa Kimeru; na ‘kupasua chungu’ kwa Kiswahili.

chungu.’<sup>26</sup> Kwanza litangazwe kwa umma wiki mbili kabla chungu hicho hakijavunjwa kwa kesi hiyo. Kutangaza kuna maanisha kumpa mtu anayehisiwa nafasi ya kujitokeza yeye mwenyewe kabla hajachelewa. Kama asipojitokeza mtaalamu wa kuvunja chungu ataitwa. Mtaalamu huyu hutumia aina fulani ya chungu kidogo cha mfinyanzi chenye alama ya kike, yaani mwanamke mwenye maziwa mawili au moja, halafu anaweka mmea fulani maalumu ndani ya kile chungu na kuombea laana kwa kusema kama mtu aliyechoma ghala, hili (au kuiba ng’ombe, au redio) hatajitokeza mwenyewe acha alaaniwe. Asipojitokeza basi laana ile itamkuta yeye na familia yake na inaweza kuleta madhara makubwa sana ikiwemo kifo. Kwa sababu hiyo mtenda maovu mara nyingi hujitokeza ili kuepusha laana (*kidengo*). Na ili kujiokoa na laana hiyo anatakiwa amlipe mtendwa kwa hatua zote za chungu na kulipa fidia ya uovu wake mapema iwezekanavyo, na akishidwa kufanya hivyo laana itamjia yeye, familia yake au wana wa ukoo wake, na pengnine vizazi vyake watakufa taratibu, au mali zake ziharibike. Uvunjaji huo wa ‘chungu’ huonekana kama ni njia rahisi kumlizimisha mtenda maovu kujitokeza hadharani na hivyo kutatua tatizi hilo.

Mazingira mengine yanayoonekana kusababishwa na kupasua ‘chungu’ ni ikiwa kama kuna mfululizo wa mikosi

---

<sup>26</sup>Utamaduni huu umeenea mbali ya Wameru ambao pia husema waliuhazima kutoka nje. Moore anataja pia tambiko la ‘kuvunja chungu’ kutoka kwa jirani zake Wachaga wa Kilimanjaro (Moore 1986: 48-49)



katika familia fulani au ukoo fulani. Watu huanza kutafuta chanzo chake na watakubalina kwamba familia hiyo au ukoo wao umefanya kitu kibaya huko nyuma. Hii inaweza kuwa ilitendeka muda mrefu uliopita na hawakulipa kwa hilo. Labda kuna mtu alikiuka miungu au mababu wa zamani na sasa wengine ndio wanalipiziwa kisasi. Labda aliuwa mtu, au aliiba kitu na hajawahi kukiri kosa baada ya ‘chungu’ kuvunjwa. Hata hivyo shida hapa huwa ni kumpata aliye husika na ni kitu gani alikosa ambacho hakikuwapendeza miungu au mababu au wale waliotendewa ubaya.

Kwa sababu laana ilihatarisha ukoo mzima wa aliye fanya makosa, hakuna mtu anayeruhusiwa kuvunja ‘chungu’ bila ruhusa kutoka katika ukoo wake. Hatari itakuwa ni kwamba muovu anatoka katika familia inayopata shida ambapo ‘chungu’ hicho kinaweza kuchochea moto na kurudisha laana kwa ukoo mzima. Ukoo unaohisiwa kwanza utaitana na kufanya majadiliano na kuhakikisha hakuna mtu ndani ya ukoo ambaye anahusika na kesi hiyo, kabla ya kuruhusu shughuli ya ‘chungu’ ifanyike. Kutokana na madhara ya vifo kwa sababu ya ‘chungu’ mwishoni mwa mwaka 1980, Wameru waliamua kuongeza sharti moja juu ya uvunjaji wa ‘chungu’ ambapo ni *Kamati ya Mringaranga* (Kabila zima) ndiyo pekee itakayotoa ruhusa ya mtu kuvunja ‘chungu.’

Wameru wengi mpaka sasa wanakubaliana na utamaduni wa kuvunja ‘chungu’ kama nja ya kusaidia jamii hasa ya kuwafanya watu wajiheshimu na wasitende maovu. Hata hivyo Wapentekoste, ambao mahubiri yao yameanza kuenea Mlima Meru<sup>27</sup> walipingana sana na utamaduni huo. Waliamini hiyo ni dhambi, na wakasema kwamba kuvunja ‘chungu’ ni kuita mapepo au mizimu kuwashambulia wakristo wenzao.<sup>28</sup>

(iii) Kama ilivyoelezwa mwanzo, wazo la ‘Katiba’ ya kikabila lilianzishwa na serikali ya Waingereza mwaka 1948 lakini haikuweza kupitishwa kwa sababu ya kesi ya Wameru. Baada ya kesi ya ardhi ya Wameru kumalizika<sup>29</sup> na mangi kujiuzulu mwaka 1952, mazungumzo kuhusu Katiba yaliendelea kati ya Waingereza na wa wakilishi wa Wameru, pamoja na wajumbe wa chama cha muungano wa Wameru yaani Meru Citizens Union. Baada ya mikutano kumi na miwili Katiba mpya iliandikwa na kuzungushwa katika jamii nzima ya Wameru. Ilijadiliwa katika mikutano ya Kijiji na hatimaye kukubaliwa mnamo Mei 27,1953. Sifa kubwa ya Katiba mpya ni kumchagua Mangi kwa kutumia kura ya siri, mgawanyo kati ya kiongozi mkuu na sheria katika matabaka yote, na kuunda

---

<sup>27</sup> Kanisa la Pentekoste lilianza Meru mwaka 1968 na likastawi wakati wa mzozo ndani ya Kanisa la Kilutheri mwaka 1990 – 1993 (Baroin 1996: 543)

<sup>28</sup> Wapentekoste pia walikataza wafuasi wao kujihusisha na *Kamati* ya kimila.

<sup>29</sup>Wameru hawakushida kesi yao ya mashamba huku New York na Wazungu wakakaa katika mashamba ya Wameru, miaka mitano baadaye Wazungu waliondoka na Wameru kuchukua mashamba tena (Puritt 1970:9-10).

Kamati ndogo ya kabila itakayohusika na kuhudumia jamii nzima.<sup>30</sup>

Baada ya Katiba mpya kupitishwa, Mangi mpya Sylvanos Kaaya alichaguliwa. Alihusika na mambo yote ya kiutawala na alihusika zaidi na utawala wa kikoloni ambapo mshili mkuu (*nshili nnini*) alibaki katika mambo ya ndani katika kabila. Mwaka 1963, mara baada ya kupatikana kwa uhuru, utawala wa kimangi ulivunjwa rasmi na Serikali. Hii ilikuwa ni pamoja na tawala zote za kichifu. Wakati huo huo Katiba ya mwaka 1953 ilifutwa na nakala yake kupotea kabisa.<sup>31</sup> Na pia haikujulikana kama ilitumika baada ya Kaaya kuchaguliwa. Hata hivyo suala la Katiba halikuishia katika mfumo wa uongozi wa *Nshili Nnini* ambaye aliendelea kufanya kazi zake. Yeye hakuweza kusitishwa kwa kuwa hakuwahi kutambulika rasmi tokea kuchaguliwa kwake.

Baada ya ukomeshaji wa mwanzo wa mfumo wa kikabila, *Nshili Nnini* na *Kamati* yake walihusika ndani ya kabila na hasa kwa mambo ya maadili katika kabila kulingana na sheria za asili za kimila, na kwa msingi huu waliweza kuamua kesi mbali mbali mpaka baadaye walipoamua kuziweka sheria hizi katika maandishi kwa kutumia muundo ule ule waliouanzisha Waingereza mwaka 1948. Lakini hata hivyo yaliyokuwamo

---

<sup>30</sup>Puritt 1970: 70.

<sup>31</sup> Mimi binasi sikuona nakala yake maktaba za Tanzania waka Uingereza; hata Bwana Henry A. Fosbrooke aliyesaidia kuiandika hakuwa na nakala nilipokutana naye mwaka 1992 akiwa mzee sana.

ndani ya andiko la Katiba yao yalikuwa tofauti kabisa na yale ya Katiba ile ya Waingereza.

Katiba hii iliandikwa kwa Kiswahili na ilikuwa na mfumo na miundo tofauti tofauti. Katika awamu nne nilizokaa Meru,<sup>32</sup> niliweza kukusanya nyaraka tofauti tofauti nne zote zikiwa ni sehemu ya Katiba hiyo, ambazo zilihusiana na kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka 1985 hadi 1995.

Nakala ya kwanza niliyopita ilikuwa ni wa mwaka 1985 ambao ulikuwa na kurasa sita zilizochapwa kwa Kiswahili, ukiwa na kichwa cha habari ‘Maamuzi ya Mkutano wa Viongozi wa Kimila wa Wameru – Awamua Tatu -1985.’<sup>33</sup> Nakala hii ilionyesha majina 14 ya Wajumbe wa Kamati ya Kabila waliotunga sheria 66 (zikiwemo sheria mpya na sheria zilizobadilishwa). Ilisainiwa na watu watatu: Yesaya Lemera Kaaya ambaye ndiye alikuwa mwenyekiti wa Kamati hiyo, mrithi wake Moses Isacki Nnko,<sup>34</sup> na Katibu wa Kamati hiyo ya Kabila.

Nakala ya pili iikuwa imeandikwa kwa Kiingereza ambapo tarehe yake ilikuwa mwezi Desemba 1986, ambayo ilikuwa na kichwa: ‘Sheria na Taratibu za Kabila la Wameru.’ Nayo ilianza na majina yale ya watu 14 ikifuatiwa na wingi wa

---

<sup>32</sup> Awamu hizi nne ziilikuwa kati ya mwaka 1992 na 1997, na wakati mwingine nilikaa hadi miezi 10.

<sup>33</sup> Hakukuwa na Nakala yoyote iliyoonyesha Awamu ya Kwanza wala Awamu ya Pili.

<sup>34</sup> Katika muda huo Yesaya alikua *Nshili Nnini*, na msaidizi wake Moses alisimikwa mwaka 1986.

aya. Ile nakala ya awali ilikuwa na kurasa 66, zikaongezeka na kuwa 74, na zikagawanyika katika vichwa vidogo vidogo: Sheria kuhusu ndoa, majeraha au mauaji, wizi wa mifugo au chakula, sheria kuhusu vifo na urithi, na sheria kuu kwa ujumla.

Nakala ya tatu ilihusiana na awamu ya 4 ya Katiba ya mwaka 1985. Iliandikwa kwa Kiswahili. Hii ilikuwa mnamo mwaka 1989, muda huu ilihusisha orodha ya sheria 81 zilizoamuliwa na Kamati ya Wajumbe 16.

Nakala ya mwisho ilikuwa makubaliano ya mnamo 1995 ya Kamati ya Wajumbe 20. Rasimu yake ya mwaka 1989 ilikuwa na kurasa kumi na mbili ikaendelezwa na kuwekwa katika kurasa safi 25 ambapo hoja 81 zilezile zimepewa maelezo zaidi. Lengo lao kubwa ni kutoa utata katika kutafsiri sharia zake. Na kichwa kilikuwa kinajitosheleza: ‘Sheria za Mila na Desturi zilizoamuliwa na Mkutano Mkuu wa Viongozi wa Wameru (Mringaringa) tarehe 28 mwezi wa kwanza 1995.’<sup>35</sup> Hata hivyo chini ya ukurasa wa mbele zimeandikwa: ‘zimetungwa na Halmashauri Kuu ya Jadi na Mila za Wameru.’

Nakala zote nne zinatuhakikishia kwamba kwa kipindi cha miaka ya hivi karibuni Wameru wamekuwa makini na utungaji wa sheria zao. Kutoka hatua moja kwenda nyingine na pole pole hatimaye Katiba ilikamilika. Ukilinganisha toka nakala ya kwanza na hata ya mwisho (1985 na 1995) inatusaidia kujua ni

---

<sup>35</sup>‘*Sheria za Mila na Desturi zilizoamuliwa na Mkutano Mkuu wa Vashili wote (Mringaringa) tarehe 28 mwezi wa kwanza 1995.*’

hatua zipi zilipitiwa na kuona kwa hakika kuwa Katiba hii imepitia hatua si haba.

### **Kuhusiana na wakati wa sasa**

Nakala zote zinaonyesha mlolongo wa faini au fidia mbali mbali zinazopaswa kulipwa katika nyakati mbali mbali. Vifungu 18 vya mwanzo vinahusika na malipo ya mahari katika ndoa ambapo vinaonesha mtiririko mrefu wa wanyama, fedha na zawadi nyingine ambazo muoaji anapaswa kutoa kwa familia ya binti atakayeolewa kabla na baada ya ndoa. Hata hivyo haujatajwa wakati sahihi ambapo vitu hivi vitatolewa. Kifungu kingine kirefu kinaonyesha aina gani ya fidia itolewe kulingana na ukubwa wakosa: majeraha ya aina tofauti, mauaji, kumtia binti ujauzito, wizi wa aina zote (mifugo, mazao ya kilimo, asali au mizinga ya nyuki). Mada nyingine maalumu ambazo zimeelezewa katika nakala hizo ni kuhusiana na urithi, kuuza au kukodisha shamba au sheria nyingine za kiuchumi kama vile zile zinazofuatwa endapo mtu anatumza mifugo au shamba la mtu mwingine.

Mchanganuo mzima wa sheria hizi ambazo Wameru wanazifuata kama ndio msingi wa mila zao, unahusisha maelezo kuhusu desturi na miiko ya jamii yao. Itakuwa vema kuyataja mabadiliko muhimu yaliyoletwa na Katiba mpya, ukilinganisha na ile iliyoandikwa miaka kumi iliyopita, ambayo

inatoa ushahidi kuhusu mabadiliko ya kijamii yaliotokea katika jamii ya Wameru.

Kutoka nakala moja kwenda nyingine sheria na taratibu zimepangwa upya katika mtiririko mzuri na hoja zingine kumi na tano zimeongezwa, kufanya Katiba mpya kuwa ndefu (kutoka vifungu 66 mpaka 81) na yenye maelezo ya kina. Sheria nyingi zimepangwa katika mpangalio mzuri na mifano imewekwa ili kuondoa utata fulani. Hii ni dalili ya kujali mpangilio mzuri na kuthamini mapendekezo ya watu katika sheria hizi.

Kitu kingine kilichozingatiwa ni kuzifanya sharia ziendane na wakati. Hii inaweza kuonekana ukichukua utofauti wa nakala hizi mbili; kwa mfano jinsi ya kulipa fidia ambapo kumeongezeka kulingana na kuongezeka kwa bei au thamani ya vitu. Pia inaonyesha jinsi watu wanavyoelewa kuhusu mfumuko wa bei na jinsi ya kushughulikia madhara yake.

Alama nyingine ya Wameru kwenda na wakati ni kule kuongeza tamko jipya linalokazia umuhimu wa wazazi kuwapeleka watoto shule za msingi na sekondari au vyo vya ufundi. Utoaji wa elimu unafaa sana katika Mlima Meru kutokana ongezeko la watu na uhaba wa aridhi. Kwa kuangalia ukata wa hali halisi imebidi Katiba kutafuta njia nyingine za kuingiza kipato ambapo elimu ilionekana kuwa ndio suluhisho.

Tatizo la ardhi katika Mlima Meru pia lilipelekea watu wafuge mifugo michache. Haitashangaza kwamba fidia nyingi zilizolipwa kwa makubaliano (ng`ombe au mifugo mingine) mwaka 1985, zimewekwa katika mfumo wa malipo ya fedha katika Katiba mpya. Watu wachache sana wangeweza kulipa aina hii ya fidia kwa njia ya vitu au mifugo kama ilivyokuwa hapo mwanzoni.

Jambo jingine linaloonyesha nia ya Kamati ya Wameru katika kubadili sheria za kimila kulingana na mazingira ya kisasa ni uamuzi wa Kamati kuweka sheria zitakazofuatwa endapo mtu atasababisha ajali ya gari. Matukio hayo ya ajali yamekuwa mengi kwa sababu ya kuwepo kwa barabara nzuri ya lami ya Arusha- Moshi kusini mwa mlima Meru na hata barabara nzuri na za lami katika baadhi ya vijiji vya Wameru.

Lakini maendeleo mengine mapya katika Nakala ya mwaka 1995 yanatokana na mabadiliko ya Wameru katika mila na desturi zao. Hapo awali watoto waliokuwa wamezaliwa nje ya ndoa walitengwa kabisa na kufikiriwa tofauti na hawakupewa haki yeyote. Katiba mpya imelichukulia hilo na kulipa uzito kama suala muhimu kwa kutoa haki ambazo hawakuwa nazo hapo awali. Mwelekeo mpya uliletwa ambao kwa kiasi ulichangiwa na uwepo wa Kanisa, na fikra kubwa imekuwa kwamba akinamama hao na watoto wao wapewe kiasi fulani cha msaada wa kijamii na kiuchumi. Kifungu kimoja



kipya katika Katiba mpya kinaeleza kwamba kama mwanaume atajulikana ndiye baba wa mtoto hata kama alimkataa mama yake, atatakiwa aendelee kuleta mahitaji ya mtoto kama vile adaa shule kama afanyavyo baba aliyeoa, na pia ampe sehemu ya urithi wake.

Zaidi ya hayo sheria nyingine mpya mahususi zinahusika na kesi za kutembea na mwanamke nje ya ndoa, na kipengele kipyaa kikawekwa ambacho kinaruhusu mabinti kurithi ardhi kutoka kwa baba zao, kama hawaishi na waume zao (tafsida ya kusema ikiwa hawajaolewa). Katiba mpya si tu inajaribu kuweka vizuri haki ya mama na mtoto, bali pia imeweka adhabu kubwa kwa mwanaume aliyempa ujauzito msichana na akakataa kumwoa. Adhabu hii kali ni alama nyingine ya kuonyesha kukua kwa kile kinachoitwa kupambana na mmomonyoko wa maadili na kutowajibika katika kabila la Wameru.

Wanawake walioolewa wanapewa haki nyingi, kwa mfano, kifungu kipyaa kinaeleza kwamba mwanamke aliyeachwa na mume wake ana haki ya kulima shamba ambalo ukoo wa mume wake watampatia. Hii ni njia ya kumpa urahisi wa kujipatia mazao ya chakula na kukaa na watoto wake katika eneo hilo. Adhabu kubwa hutolewa kwa mume aliye mjeruhi

mke wake na kumvunja mfupa mmojawapo wa mwili wake ambapo mbuzi jike ameongezwa katika faini ya mwanzo.<sup>36</sup>

Wakati ambapo vifungu vingi katika katiba ya Wameru vinaelekea kujali hali ya kisasa, vifungu vingine bado vimebakia zaidi katika mambo ya kimila, kwa mfano, mila za ‘kuvunja chungu’ zimebaki vile vile isipokuwa wameweka sharti kwa kusema kwamba hairuhusiwi kuvunja ‘chungu’ bila ruhusa ya *Kamati*. Hata hivyo lengo la sharti hili si kutukuza desturi hii bali ni kutoa mwongozo katika utendaji wa zoezi hili la hatari.

Mbali na mambo yote yaliyomo katika nakala hizi, ardhi imeonekana kuwa msingi mkubwa katika toleo jipya ambapo vifungu vingine viwili kuhusiana na ardhi viliongezwa. Kimoja kinaelezea nini kifanyike ikiwa mtu kwa bahati mbaya amevuka mpaka wa shamba lake (ikitokea mara nyingi), na kifungu cha pili kinakataza kuweka shamba rehani kwa ajili ya kupewa mkopo. Kifungu hiki kinachukuliwa kama ni wazo la wazee (ambao wengi wao wako katika *Kamati*) ambao mara nyingi hulinda ardhi ambayo ndiyo inayoonekana kama rasilimali muhimu katika jamii ili isije ikauzwa kinyemela kwa kuiweka rehani na kuiuza bila ruhusa kutoka katika ukoo husika.

---

<sup>36</sup> Mnamo mwaka 1985, ng’ombe mmoja, mbuzi mmoja, na bia kwa ukoo zote mbili ziliongezwa.

Vifungu vingine zaidi vilivyoongezwa vinahusika zaidi na haki za kikatiba. Wanaelezea jinsi gani *Nshili* anatakiwa achaguliwe ambapo imewekwa wazi kwamba ni marufuku kwa kiongozi kuhodhi madaraka. *Nshili* wa ukoo hatakiwi kuwa kiongozi wa Kanisa wala wa rika lolote.

Sifa nyingine ya mwisho ya rasimu ya nakala ya mwaka 1995, ni kule kutambua mamlaka ya juu yaani Serikali ya nchi. Hili limethibitika pale ambapo katika kifungu cha mwisho baada ya kutaja majina 20 ya wajumbe wa Kamati ya Katiba ambao walipitisha mswada walipoweka maandishi katika sentensi moja kuonyesha kibali cha serikali: ‘Kama ilivyothibitishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.’<sup>37</sup> Nafasi wazi ikaachwa kwa mwana sheria huyu kusaini.

Katiba hii kwa ujumla, kama ilivyoelezwa hapo awali, imepitia hatua zifuatazo:

- > Katiba mpya iliandaliwa na Kamati ya *Vashili* ambao majina yao yametajwa mwishoni.
- > Halafu ikajadiliwa kwa kina na kupitishwa na viongozi wa ukoo na viongozi wa rika.
- > Halafu ikapelekwa kupewa kibali na Serikali ya Tanzania kama sentensi ya mwisho katika waraka wa 1995 inavyothibitisha.

---

<sup>37</sup> Zimeidhinishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Hakika Wameru waliona kwamba Katiba yao haitohibitika ikiwa kifungu chochote kilichoko katika Katiba hiyo kitapingana na sheria za nchi. Hii inaonyesha ni kwa kiasi gani Wameru wanajiona kuwa ni sehemu ya Watanzania, mtizamo ambao umeenea karibu nchi nzima. Wakati wa utafiti wangu Wameru walikuwa wakisubiri jibu zuri kutoka Serikalini kabla ya kuitisha mkutano wa kuidhinisha rasmi Katiba yao. Ni hapo tu ndipo wangeanza kuitumia kama sheria yao mpya. Kwa wazo hilo katika fikra zao ni ukweli tosha kwamba hakuna lugha ambayo itatumika zaidi ya Kiswahili au Kiingereza kama lugha rasmi, na inayoeleweka kote Tanzania.

### **Hitimisho**

Katiba ya Wameru imeonyesha ni picha ya jinsi Wameru wamejikea kama msingi wa sheria zao za asili. Japo sheria hizi ni zile ambazo Wameru wanataka zitumike na wao wenyewe au zitumike kwao tu bado wanaweza wasifikie hatua ya utekelezaji wa sharia zote. Hata Moore aligundua tatizo hili kulinganishana sheria na desturi za Wachagga akisema: ‘kufuata kikamilifu matakwa ya sheria mara nyingi hulegalega.’<sup>38</sup> Kwa mfano mifugo ambayo mtu anayeoa anatakiwa kutoa kwa wakwe zake mara nyingine hulipwa mwaka mmoja baadaye au hata zaidi.

---

<sup>38</sup> Moore 1986: 40.

Mfano, kijana mmoja aliniambia kwamba siku chache tu zilizopita alilipa mahari badala ya baba yake ambaye alifariki bila ya kumalizia kulipa mahari hiyo. Kuna ukweli kwamba sheria wakati mwingine zimekuwa hazifuatwi wala kutiliwa mkazo. Lakini mara nyingi wakati matatizo au majanga yanapotokea sababu zinazotolewa huwa ni kulegalega au kushindwa kuzitii sheria.

Katiba si tu kwamba inatoa mwanga juu ya jinsi Wameru wanavyoutazama utamaduni wao, bali pia inasaidia kama sera na mipango. Kwa kuiweka katika maandishi na vyombo vya kiutawala, Katiba yao ni utambulisho kuwa Wameru wumetengeneza na kuimarisha taratibu zao. Katika historia taasisi za kikabila zilizoelezwa katika toleo hili ziliundwa ili kuupinga utawala wa Waingereza, mfano katika Kesi ya Ardhi ya Meru. Lakini pia inaweza kueleweka kama ni matokeao ya ule utawala wa kutumia mangi wa Waingereza ambao ulilenga kurahisisha utawala wao. Iliffe akasema kwamba kwa mtizamo wake Waingereza waliona kwamba Waafrika wamegawanyika katika makabila mbali mbali kwa hiyo waliimarisha hali hiyo ya utengano ili waweze kufanya kazi vizuri katika mfumo wa kikoloni na kufanikiwa kutawala kirahisi.<sup>39</sup>

Taratibu za kiutawala za Wameru zinaonyesha hamu yao kuu ya kujiona kama ni kabila lenye mshikamano, na kwa njia hiyo

---

<sup>39</sup> Iliffe 1979: 318.

mtu hatashangaa kuona walivyoweza kwa kiasi kikubwa kuzibadili mila na sheria zao ili ziendane na mfumo wa kisasa jambo ambalo halionekani sana katika jamii nyingi za Kiafrika isipokuwa kwa makabila machache tu.<sup>40</sup> Hata hivyo umoja wa Wameru ulitikisika mwanzoni mwa mwaka 1990 wakati wa vurugu zilizotokana na mzozo wa nani amiliki dayosisi ya Kilutheri eneo la Mlima Meru.<sup>41</sup> Mgogoro huo ulikuwa kati ya uongozi wa Kanisa la Kilutheri kwa upande mmoja, na watu walio hasi kanisa hilo ambao baadaye walianzisha kanisa jingine. Hii illipelekea machafuko ya kijamii kiasi kwamba mipango ya maendeleo iliyokuwa imewekwa haikuweza tena kutimizwa. Mbaya zaidi mpango kazi mzima wa taasisi za kiutawala za Wameru haukuweza kufikiriwa tena. Katika jamii ya Wameru ya sasa, mila na vyombo vya kiutawala vinakumbana na vyombo vingine viwili vya kiutawala ambavyo ni Kanisa na Serikali ya nchi.

## **Marejeo ya vitabu**

BAROIN, Catherine. 1996. Religious conflict in 1990-1993 among the Rwa: secession in a Lutheran diocese in Northern Tanzania. *African Affairs*, 95, n° 381: 529-554.

BAROIN, Catherine. 1998. Introduction et culture du café chez les Rwa de Tanzanie du Nord. In: CHASTANET, Monique (éd), *Plantes et paysages d'Afrique. Une histoire à explorer*, Paris : Karthala & ORSTOM, 529-549.

---

<sup>40</sup> Angalia kwa mfano Nkoya wa Mangaribi mwa Zambia (van Binsbergen 1992), au Ngwato wa Mashariki mwa Botswana (Landau 1995).

<sup>41</sup> Baroin 1996: 540-550.

- BAROIN, Catherine. 2001. De la bière de banane au soda en bouteille. Religion et boisson chez les Rwa du Mont Meru (Tanzanie du Nord). *Journal des africanistes*, 71-2: 77-94.
- CORY, Hans. Cory Paper n° 71. Dar-es-Salaam: University Archives.
- ILIFFE, John. 1979. *A Modern History of Tanganyika*, Cambridge: Cambridge University Press.
- JAPHET, Kirilo & SEATON, Earle. 1967. *The Meru Land Case*. Nairobi: East African Publishing House.
- JOHNSON, Frederick. 1971. *A Standard Swahili-English Dictionary*. Oxford: Oxford University Press (reed. 1990).
- LANDAU, Paul S. 1995. *The realm of the word: Language, gender and Christianity in a southern African kingdom*. London: Currey.
- LUANDA, Nestor N. 1986. "European commercial farming and its impact on the Meru and Arusha peoples of Tanzania, 1920-1955". Ph. D. Thesis, University of Cambridge.
- MOORE, Sally F. 1986. *Social facts and fabrications. "Customary" law on Kilimanjaro, 1880-1980*, Cambridge: Cambridge University Press.
- PURITT, Paul. 1970. "The Meru of Tanzania: A study of their social and political organization", Ph. D. Thesis, University of Illinois.
- SPEAR, Thomas. 1997. *Mountain Farmers. Moral Economies of Land and Agricultural Development in Arusha and Meru*. Oxford: James Currey / Dar-es-Salaam: Mkuki na Nyota / Berkeley: University of California Press.
- Tanganyika Territory, *Annual reports of the provincial commissioners, 1929-1959*. Dar-es-Salaam: Government printer.
- Tanganyika, 1954. "Local government Memoranda", n° 1, part 1, Dar-es-Salaam: Government Printer.
- van BINSBERGEN, W.M.J. 1992. *Tears of rain: Ethnicity and history in Central Western Zambia*. London: Kegan Paul.
- van ROUVEROY van NIEUWAAL, E.A.B. 1992. The Togolese chiefs: Caught between Scylla and Charibdis? *Journal of Legal Puralism and Unofficial Law*, 32: 19-46.
- van ROUVEROY van NIEUWAAL, E.A.B. 1996. State and chiefs: Are chiefs mere puppets? In: RAY, D.I. & van ROUVEROY van NIEUWAAL, E.A.B. (eds), The new relevance of traditional authorities to Africa's future, in: *Journal of Legal Puralism and Unofficial Law*, 37-38:39-78.
- van ROUVEROY van NIEUWAAL, E.A.B. 1999. Chieftaincy in Africa: Three facets of a hybrid role. In: van DIJK, R. & van ROUVEROY van NIEUWAAL, E.A.B. (eds), *African chieftaincy in a new socio-political landscape*. Hamburg/Münster: LIT Verlag, 21-47.